

## **TAARIFA YA KITENGO CHA KAMPENI YA KITAIFA YA USAFI WA MAZINGIRA**

**UTANGULIZI:** Wilaya yetu inatekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira katik avijiji vyote vya wilaya. Kampeni hii inafanyika nchi nzima ambapo kila kaya, Taasisi,maeneo ya biashara, ofisi na maeneo yote ya umma yanatakiwa kuwa na vyoo bora na kuzingatia matumizi yake kwa usahihi. ujenzi wa vyoo bora unaenda sambamba na kuweka vifaa vya kunawia mikono na sabuni kwa ajili ya kunawa baada ya kutoka chooni. Kwa kuwa Kampeni hii itahusisha vijiji vyote vilivyo katika wilaya yetu ya Ngara, viongozi na wadau wote wanapaswa kuzingatia maelekezo yote muhimu kwa mitaa na Vijijivyo vinapaswa kuanza uhamasishaji wa watu wake ilikujenga na kuboresha vyoo walivyonyavyo, ilikuuhakikisha kuwa kila kaya inakuwana choo bora nakukitumia ipasavyo.

### **MALENGO:**

- Kulinda afya ya jamii kwa kuboresha usafi wa mazingira ulio endelevu.
- Kuimarisha ubora na ufanisi katika utoaji wa huduma za kinga ili kuzuia maradhi na ulemavu na hivyo kupunguza vifo na gharama za kutibu magonjwa.

### **MAFANIKIO:**

- Kaya zipatazo 34,181(59%) zimeweza kujenga vyoo bora na kuvitumia
- Viongozi wa vijiji 66 vya wilaya ya Ngara wameweza kuhamasishwa juu ya kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira
- Kutokuwepo magonjwa ya mripuko ndani ya wilaya yatokanayo na uchafuzi wa mazingira

### **HALI HALISI YA VYOO**

IDADI YA KAYA(W)	KAYA ZILIZO TEMBEL EWA	KAYA ZENYE VYOO BORA	KAYA ZENYE VYOO VYA	KAYA ZISIZO NA VYOO	KAYA ZENYE VYOMBO VYA KUNAWIA MIKONO BAADA YA KUTOKA CHOONI	KAYA ZISIZO NA VYOMBO VYA KUNAWIA MIKONO BAADA YA KUTOKA CHOONI
71,803	57,934	34,181(59%)	23,149(39.9%)	604(1.1%)	8,111(14%)	49,823(86%)

### **CHANGAMOTO**

1. Upungufu mkubwa kwa watumishi kwa kada ya maafisa Afya wasaidizi (kata 5 kati ya 22 ndo zenyne maafisa afya wasaidizi)
2. Kaya nyingi kutoona umuhimu wa ujenzi wa vyoo bora
3. Bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli ya usafi wa mazingira

## **MIKAKATI/UTATUZI**

- Viongozi wa kata,vijiji na wataalam waliopo ngazi ya kata kuhakikisha wanasi mamia kaya zote zinajenga vyoo na kuvitumia sambamba na unawaji wa mikono kwa sabuni kwa maji tiririka baada ya kutoka chooni
- Kuendelea kutoa elimu juu ya ujenzi wa vyoo bora kuitia mikutano ya wananchi wote na kutumia radio iliyo hapa wilayani(Radio Kwizera)
- Kuendelea kushirikiana na washitiri(partners)waliopo wilayani wanohusika na shughuli za usafi wa mazingira
- Matumizi ya sheria ndogo za vijiji kuwajibisha wasaiotekeliza na kufuata kanuni za afya.
- Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaimarisha utoaji wa elimu ya afya, ili kumhamasisha na kumwezesha kila mtu kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya na maisha bora.
- Halmashauri kwa kushirikiana na wadau itaandaa sharia ndogo, miongozo na mikakati ambayo itakayowezesha kila mtu kupata elimu, ili kulinda, kukuza na kuendeleza afya bora.

Imeandaliwa na :

### **WADAU WANAO TOA HUDUMA ZA AFYA (PPP)**

**Utangulizi:** Katika kuhakikisha kuwa wananchi wana afya bora, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa huduma za afya kwa kuzingatia sera na miongozo iliyopo. wilaya ya Ngara inashirikiana na wadau mbali mbali kutoa huduma za Afya kwa wananchi

### **Malengo:**

- Kutoa huduma muhimu za afya zenyne uwiano wa kijiografia,viwango vya ubora unaokubalika, gharama nafuu na zilizo endelevu.
- Kujenga ushirikiano kati ya sekta ya umma, sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kijamii na jamii katika kutoa huduma za afya.

**Mafanikio:** uwepo wa wadau na kusaidia kutoa huduma za afya wilayani Ngara

## CHANGAMOTO

1. Wadau kuja na malengo ya kusaidia katika maeneo maalum
2. Kukidhi matarajio ya wananchi kwa kuwa na huduma bora za afya
3. Bajeti za utekelezaji kutokuwa wazi na gharama halisi ya miradi kutofahamika kwa halmashauri ya wilaya
4. Vikao vya kila robo na wadau wanaotoa huduma za Afya kushindwa kufanyika kutokana kutokuwepo bajeti maalum.

### Utatuzi wa changamoto-

Kuhitisha vikao na wadau wote wa huduma za Afya na kukubaliana kwa pamoja namna ya kuboresha huduma za Afya zitolewazo kwa wananchi

### WADAU WA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA AFYA WILAYA YA NGARA

S/N	JINA LA MDAU WA MAENDE LEO	JINA LA MRADI	MTEKELEZAJI MKUU	ENEO LA KIPAUMBE LE LA MRADI	NGAZI YA UTEKEL EZAJI YA MRADI	MKOA	HALMA SHAURI	KATA	KIJIJ	ZAHANATI
1	ANGLICAN CHURCH-DIOCES OF KAGERA	HOSPITALI TEULE YA MURGWANZA	ANGLICAN CHURCH-DIOCES OF KAGERA	HUDUMA ZA AFYA TIBA NA KINGA	KAGERA	NGARA	22	75		
2	ROMAN CATHOLIC CHURCH	HOSPITALI YA RULENGE	ROMAN CATHOLIC CHURCH	HUDUMA ZA AFYA TIBA NA KINGA	KAGERA	NGARA	9	24		

3	ROMAN CATHOLIC CHURCH	LOURDES DISPENSARY	ROMAN CATHOLIC CHURCH	HUDUMA ZA AFYA TIBA NA KINGA	KAGERA	NGARA	2	4	1
4	ROMAN CATHOLIC CHURCH	BUHORO RO DISPENSARY	ROMAN CATHOLIC CHURCH	HUDUMA ZA AFYA TIBA NA KINGA	KAGERA	NGARA	2	10	1
5	CSI/IMA WORLD HEALTH	NEGLECTED TROPICAL DISEASES	NTDCP/WIZARA YA AFYA	MAGONJWA YASIYOPE WA KIPAUMBEL E	KAGERA	NGARA	22	75	0
6	USAID	ICAP-ENDELEZA PROJECT	ICAP/NGARA DC	KUDHIBITI MAAMBUKI ZI YA VIRUSI VYA UKIMWI	KAGERA	NGARA			
7	USAID	AFRICA AIRS	ABT/DED	UPULIZIAJI DAWA YA UKOKO MAJUMBANI(IRS)	KAGERA	NGARA	22	75	0
8	TUMAINI HEALT CENTER	TUMAINI HEALT CENTER	MMILIKI TUMAINI HEALT CENTER	HUDUMA YA TIBA KWA WAGONJWA	KAGERA	NGARA	3	9	0
9	KABANGA PRIVATE DISPENSARY	KABANGA PRIVATE DISPENSARY	MMILIKI KABANGA PRIVATE DISPENSARY	HUDUMA YA TIBA KWA WAGONJWA	KAGERA	NGARA	1	6	1

10	USAID	BORESH A AFYA	USAID/HW	HUDUMA ZA AFYA YAMAMA NA MTOTO	KAGERA	NGARA	22	75	54
11	USAID	KUDHIBI TI MAAMB UKIZI YA VIRUSI VYA UKIMWI	MDH	KUDHIBITI MAAMBUKI ZI YA VIRUSI VYA UKIMWI	KAGERA	NGARA	12	58	15
12	USAID	TAKWIM U ZA UZAZI WA MPANGO	CHAI	TAKWIMU ZA UZAZI WA MPANGO	KAGERA	NGARA	22	75	50
13	JEPHGO	HUDUM A ZA AFYA UZAZI NA MTOTO	JEPHGO/NGAR A DC	HUDUMA ZA AFYA YAMAMA NA MTOTO	KAGERA	NGARA	22	75	54
14	ENGENDE R HEALTH	UZAZI WA MPANGO	ENGENDER HEALTH	UZAZI WA MPANGO	KAGERA	NGARA	22	75	54
15	USAID	LISHE BORA KWA MTOTO	IMAS/DED	LISHE BORA KWA MTOTO	KAGERA	NGARA	22	75	54
16	USAID	UZAZI WA MPANGO	PSI/NGARA DC	UZAZI WA MPANGO	KAGERA	NGARA	22	75	51

18	CCBRT	CLEFT PARATE REPAIR/F ISTURA	CRBRT	CLEFTPARA TE REPAIR	KAGERA	NGARA	22	75	61
19	KABANG A NICKEL	KUNUNU A DAWA NA VIFAA TIBA	KABANGA NICKEL	KUNUNUA DAWA NA VIFAA TIBA	KAGERA	NGARA	4	12	3
21	USAID	CHANDA RUA KLINIKI	JOHN HOPEKINS UNIVERSITY	UGAWAJI WA VYANDARU A KWA WATOTO	KAGERA	NGARA	22	75	52
22	CARITAS	UDHIBITI WA MAABUK IZI YA UKIMWI	CARITAS	UDHIBITI WA MAABUKIZI YA UKIMWI	KAGERA	NGARA	6	9	0
24	USAID	SHUGHU LI ZA UZAZI WA MPANGO	MARIE STOPES/DED	UZAZI WA MPANGO	KAGERA	NGARA	22	75	52
25	USAID/TC DC	UDHIBITI WA MALARI A NA UKIMWI	SOCIAL ACTION PATH ORGANIZATION(SAPO)	UDHIBITI WA MALARIA NA UKIMWI	KAGERA	NGARA	22	75	0

## **KITENGO CHA UTHIBITI UBORA WA VYAKULA, DAWA NA VIPODOZI (TFDA)**

**UTANGULIZI:** Kwa mujibu wa sheria ya chakula,Dawa na vipodozi,sura ya 219,udhibiti wa usalama,ubora na ufanisi wa vyakula,dawa,vipodozi na vifaa tiba uliwekwa chini ya mamlaka ya chakula na dawa(TFDA)

Ilikuwezesha utekelezaji wa sheria hii wizara yenyewe dhamana ilikasimu baadhi ya mamlaka na majukumu ya TFDA kwa mamlaka ya serikali za mitaa kutekeleza majukumu ya TFDA kupitia GN NO.162 za mwaka 2006 na marekebisho yake kupitia GN.NO 165 za mwaka 2007.Wilaya ya Ngara inatekeleza majukumu yaliyokasimishwa kwa kuzingatia kanuni mpya kupitia GN NO.476 ya 2015 na marekebisho yake kupitia GN NO.19 ya mwaka 2017 pamoja na mwongozo ambavyo vyote vinazingatiwa katika utekelezaji.

**Malengo:**Kulinda afya ya jamii kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya chakula,dawa,vipodozi na vifaa tiba.

Mafanikio:

- Kufuata misingi ya kazi katika uwajibikaji
- Kudhibiti vyakula vyenye athari kwa watumiaji
- Kuedelea kusajiri majengo ya vyakula yenyewe sifa
- Kutoa elimu kwa wadau husika
- Ukusanyaji wa fedha za usajili na utoaji wa vibali kwa biashara ya vyakula/vinywaji

### **Changamoto**

- Uanzishwashaji holela wa biashara ya vyakula kwa maeneo yasiyo rasmi
- Upungufu wa wakaguzi wa vyakula katika maeneo mbali mbali wilayani
- Wafanyabiashara wengi kutokuwa na elimu ya utambuzi juu ya bidhaa inayofaa na isiyofaa kwa matumizi ya binadamu hususani bidhaa zilizoisha muda wake
- Kuwepo kwa baadhi ya wafanya biashara wanaopitisha au kuingiza bidhaa bandia na zilizokwisha muda wa matumizi kwa kutumia njia za panya katika mipaka yetu ya wilaya na nchi jirani.

### **Utatuzi wa changamoto:**

- (i) Halmashauri ya wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaimarisha utoaji wa elimu ya afya, ili kumhamasisha na kumwezesha kila mtu kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya na maisha bora.
- (ii) Kuendelea kutumia sheria za udhibiti wa vyakula ,dawa na vipodozi